# Maswali

1. Mungu aliahidi watu wake nini?
2. Nini ilifanya kwa taifa la Israeli?
3. Nehemia alikuwa nani?
4. Alitaka kufanya nini?
5. Mbona alipata alichotaka?
6. Nehemia alifanya nini alipofika Yerusalemu?
7. Maafisa walifanya nini?
8. Ukuta ulijengwa namna gani?
9. Mbona adui wao hawakufaulu?
10. Watu walifanya nini ukuta ulipomalizika.

# Majibu

1. Mungu aliahidi watu wake kwamba wakimtumikia atawalinda.
2. Taifa la Israeli lilishambuliwa na mataifa mengine. Mungu hakuwasaidia kwa sababu hawakumtumikia kwa hivyo walifanywa watumwa.
3. Nehemia alikuwa Myahudi na alifanya kazi kwa mfalme wa Uajemi.
4. Nehemia alitaka Mungu amtumie kujenga ukuta wa mji wa Yerusalemu.
5. Mungu alimpa Nehemia alichotaka kwa sababu alimuomba.Nehemia aliomba kwamba atamtumikia, kwa hivyo Mungu alikubali.
6. Nehemia alipofika Yerusalemu alizunguka usiku akiangalia ukuta wa mji kwa siri.
7. Maafisa walijaribu kuzuia Nehemia na wayahudi wasijenge mji tena. Waliwacheka.
8. Watu walifanya kazi kwa sehemu mbali mbali ukutani. Walisaidiana na wakafanya ukuta ukawa wa nguvu.
9. Adui wa Waisraeli hawakufaulu kwa sababu Waisraeli walikuwa na Mungu. Walimuomba awasaidie.
10. Ukuta ulipomalizika, watu wote walikusanyika ili wazikilize Ezra akisoma sheria za Mungu. Waliahidi kwamba watamtumikia Mungu vyema.

## SHULE YA JUMAPILI YA CBM

**Awamu ya 1    Mwaka wa 2**

# 28 Nehemia

## Marejeo

Nehemia 1

## Kiini cha somo

Kuonyesha kuwa twaweza kufanya lolote tukisaidiwa na Mungu

## Maneno maalum

1. Mungu + ahadi + wafalme waovu + watumwa + Koreshi + rudi.
2. Nehemia + Wayahudi waumia Yerusalemu + omba + huzunika.
3. Nehemia + omba + rudi + jenga tena + mfalme anakubali.
4. Maafisa wanavuka + Nehemia + siri + ukuta wabomoka + malango za chomwa.
5. Wayahudi + jenga tena + Sanbalati + Tobia + cheka.
6. Kila mtu alisaidia + ukuta wa nguvu + njia za utawa.
7. Sanbalati + Tobia + ghadhabika + Waisraeli waomba + linda + silaha + msiogope + siku 52.

**28.1** Mungu aliahidi watu wake kwamba wakimtumikia, atawalinda. Lakini wafalme wa Israeli walikuwa waovu sana na waliabudu sanamu badala ya Mungu. Manabii wa Mungu walikuwa wakiwaonya wakiwambia kitakachofanyika lakini walipuuza. Mataifa mengine yakashambulia Israeli na watu wengi walichukuliwa kama watumwa. Baada ya miaka 70, mfalme Koreshi wa Uajemi aliwaachilia wengine warudi Israeli. Lakini mataifa yaliyozunguka Israeli waliwachukia na waliwateza sana.

**28.2** Baada ya miaka tisini, Nehemia alimfanyia kazi mfalme Artashasta wa Uajemi. Nehemia alikuwa myahudi. Siku moja alikutana na marafiki wake waliokuwa wamerudi Yerusalemu. Walimwambia vile Wayahudi walikuwa wanateseka tena mji ulikuwa umeharibika. Alikasirika na akaomba kwamba Mungu amtumie aende asaidie Yerusalemu. Mfalme alimuona Nehemia na huzuni na akamuuliza sababu.

**28.3** Nehemia alimwambia mfalme, “Mji wa baba zangu umeharibika!” Mfalme akamuuliza, “unataka ufanye nini?” Haraka haraka akaomba Mungu halafu akauliza mfalme kama anaweza kurudi Yerusalemu na aujenge tena. Mfalme alikubali na hata akampa miti ya kutumia. Tena alimpa barua ili apelekee maafisa waliokuwa kule. Mungu alikuwa amekubali matakwa ya Nehemia. Sasa Nehemia anaenda kumtumikia Mungu.

**28.4** Nehemia aliondoka kurudi Yerusalemu. Alipofika, maafisa waligadhabika sana kuona kwamba kuna mtu atakayelinda nchi na watu wa Israeli. Walikuwa wanafurahia kufanya lolote walilotaka. Kwa siri Nehemia alizunguka kuangalia Yerusalemu usiku. Aliona kwamba ukuta uliozunguka mji ulikuwa umebomoka. malango zilikuwa zimechomwa.

**28.5** Aliwakusanya Wayahudi pamoja na akawaambia, “Ni lazima tuujenge ukuta wa Yerusalemu ndio tusiwe wanyonge tena.” Aliwambia kwamba mfalme anatuunga sisi mkono na wote wakakubali kuanza kujenga. Lakini maafisa, Sanbalati, Tobia na Geshemu waliwachekelea. Nehemia aliwambia, “Mungu ako na sisi- tutashinda. Nyinyi sio wenyeji wa hapa.”

**28.6** Kila mtu alisaidia kujenga ukuta wa mji. Makuhani, watu tajiri na maskini, wanaouza mawe ya dhamana, maafisa wa uyahudi na Walawi wote walifanya kazi kwa nafasi mbali mbali. Hawa wote wangejenga ukuta wa nguvu tena. Nehemia aliona kwamba watu wanafanya kazi kwa utawa.



**28.7** Sanbalati, Tobia na mataifa mengine waliona vibaya. Walidharau ukuta uliojengwa na Waisraeli. Walipanga kuuvunja ili ujenzi usiendelee. Lakini Waisraeli waliomba Mungu na wakapanga vile watajilinda. Nehemia aliposikia mpango wa hao adui wao, aliwapa watu wake silaha na kuwambia, “msiogope! Kumbuka Mungu ni waajabu na ni wa nguvu!” Nusu ya watu walishika silaha na nusu wakaendelea kujenga ukuta. Walikuwa na tarumbeta za kupiga kuwahatarisha.Mungu alikuwa na wajenzi. Walifanya bidii sana na wakamaliza kwa siku 52.

**28.8** Sanbalati na Tobia walijaribu kutisha Nehemia kwa njia nyingi lakini hawakufaulu. Mungu alikuwa na Waisraeli. Ukuta ulipomalizika, watu walikusanyika pamoja. Kuhani Ezra aliwasomea sheria zote zenye Mungu alipea Musa. Watu wote waliabudu Mungu na wakaahidi kumtumikia vyema. Asili mia kumi ya watu warudi kuishi Yerusalemu na kutumia Hekalu kwa kuabudu Mungu tena.